



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA
KOROGWE**



Mtaa wa Majengo, Barabara ya Moshi, S. L. P. 615 Korogwe –Tanga, Simu: 027- 2650050
Nukushi: 027- 2650075 Barua Pepe: info@korogwetc.go.tz Tovuti: www.korogwetc.go.tz

Kumb.Na. HMK/B.2/02A/133

24/05/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Mji Korogwe imepokea kibali cha ajira mpya chenye Kumb.Na. **FA.97/228/01/09** cha tarehe **13/05/2022** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora cha kuajiri nafasi za kada mbalimbali. Hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Korogwe anawatangazia watazania wote wenye sifa na ambao wako tayari kufanya kazi katika Halmashauri ya Mji Korogwe kutuma maombi kwa nafasi za kazi zifuatazo:-

1. MTENDAJI WA MTA A DARAJA LA III – TGS B (NAFASI 2)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au sita (VI) na mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA MTA A.

- i. Katibu wa Kamati ya Mtaa
- ii. Mtendaji Mkuu wa Mtaa.
- iii. Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- iv. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa.
- v. Msimamizi wa Utekelezaji wa Sheria ndogo ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- vi. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
- vii. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na Umasikini katika Mtaa.
- viii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- ix. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa na
- x. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

2. MTENDAJI WA KIJJI DARAJA LA III – TGS B (NAFASI 12)

2.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au sita (VI) na mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

2.3 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJJI.

- i. Afisa Masuuli wa Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji

